

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI

Telegramu "NISHATI".
Simu Namba: +255 26 2322018
Nukushi: +255 26 2320148
Barua pepe: ps@nishati.go.tz



Mji wa Serikali-Mtumba,
Mtaa wa Nishati,
S. L. P. 2494,
40474 DODOMA.

Kigoma

18 Septemba, 2024

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

**DKT. BITEKO MGENI RASMI HAFLA YA UWEKAJI JIWE LA MSINGI MRADI WA UJENZI
BWAWA LA KUZALISHA UMEME KATIKA MTO MALAGARASI 49.5 MW, NJIA YA
KUSAFIRISHA UMEME MSONGO WA KV 132 IGAMBA-KIDAHWE NA KITUO CHA
KUPOZA NA KUSAMBAZA UMEME CHA KIDAHWE**

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe.Dkt. Doto M. Biteko, Septemba 19, 2024 anatarajia kuwa mgeni rasmi katika hafla ya uwekaji jiwe la msingi katika mradi wa ujenzi wa bwawa la kuzalisha umeme katika Mto Malagarasi wa megawati 49.5, njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa Kilovoti 132 kutoka Igamba hadi Kidahwe yenye urefu wa Kilomita 54 na Kituo cha kupoza na kusambaza umeme msongo wa kilovoti 400/220/132/33 cha Kidahwe mkoani Kigoma.

Utekelezaji wa mradi wa Malagarasi, utagharimu jumla ya Dola za Marekani milioni 144.14 (sawa na shilingi za Tanzania bilioni 388) ambapo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itagharamia kiasi cha Dola za Marekani milioni 4.14 na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) inagharamia kiasi cha Dola za Marekani milioni 140 kama mkopo wenye masharti nafuu.

Mradi utahusisha sehemu kuu tatu ambapo sehemu ya kwanza itahusisha Ujenzi wa Bwawa la kuzalisha umeme ikiwemo tuta (*Dam*), njia za kuitisha maji (*Waterways*), jumba la mitambo ya kufua umeme (*Powerhouse*) lenye uwezo wa kuzalisha Megawati 49.5 pamoja na kituo cha kupokea umeme na kuuongezea nguvu wa msongo wa kilovoti 132 (*Switchyard*);

Sehemu ya pili inahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa Msongo wa kilovoti 132 (*Transmission Line*) yenye urefu wa km 54 ambayo itaunganisha Kituo cha kuzalisha umeme na Gridi ya Taifa kuititia kituo cha kupoza umeme cha Kidahwe;

Na sehemu ya tatu inahusisha ujenzi wa mtandao wa usambazaji umeme katika vijiji saba (7) vinavyopitiwa na mradi ambavyo ni Mazungwe, Kidahwe, Mwamilia, Kalenge, Kazuramimba, Mlela na Igamba.

Mradi wa Malagarasi unatarajiwa kuzalisha umeme wa wastani wa Gigawati hour 181 kwa mwaka. Umeme huu utasaidia mahitaji ya ndani ya mkoa wa Kigoma, mikoa ya jirani pamoja na kuwezesha biashara ya umeme kikanda (Southern and Eastern Africa Power Pools), pamoja na kuboresha huduma za kijamii ikiwemo Elimu, Afya, maji pamoja na biashara za viwanda.

Imetolewa na;



Neema Chajila Mbuja,

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini.

WIZARA YA NISHATI